**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA TISA**

**Kikao cha Sita – Tarehe 6 Novemba, 2007**

*(Mkutano Ulianza Saa 3.00 Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

**MASWALI NA MAJIBU**

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge kabla ya kumwita Mbunge ambaye atauliza swali la kwanza kwa siku ya leo, chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Napenda kuchukua nafasi hii kukipongeza sana Chama cha Mapinduzi (CCM) kwa Mkutano wake Mkuu uliofanyika siku mbili zilizopita na kuweza kutoka na ushindi mkubwa sana. Kwanza kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi (CCM), kwa kipindi kingine cha miaka mitano. Makamu wake wote wawili na mwingine akiwa aliyekuwa Spika wa Bunge hili Tukufu, ndiye Makamu mpya wa Chama cha Mapinduzi (CCM). *(Makofi)*

Pia nachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu ambaye naye ameibuka kwa ushindi mkubwa sana kwenye Mkutano huo pamoja na wengine wote waliogombea pamoja na mimi, tunajipongeza sana. *(Makofi)*

Nadhani tumeshapata Ari Mpya, Nguvu Mpya na Kasi Mpya ya kuweza kutenda mambo ya siasa ya Amani, siasa ya Umoja, siasa ya Upendo na siasa ya Maendeleo. *(Makofi)*

Na. 72

**Utekelezaji wa Ahadi za Rais**

**MHE. HAJI JUMA SEREWEJI** aliuliza:-

Kwa kuwa, kila Rais hukaa vipindi viwili (miaka kumi) kwenye Madaraka ya Urais; na kwa kuwa, Marais hutoa ahadi mbalimbali nchini:-

(a) Je, Rais anayeshika madaraka baada ya Rais mwingine kumaliza muda wake, hutekeleza ahadi hizo?

(b) Kama hazitekelezwi, Je, Serikali haioni kuwa, haiwatendei haki wananchi waliopewa ahadi hizo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. DR. BATILDA S. BURIAN)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi kabla ya kujibu swali hili, naomba nitoe pongezi zangu za dhati kabisa kwa viongozi wetu wa Chama cha Mapinduzi walioshinda katika uchaguzi uliokwisha jana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Haji Juma Sereweji, Mbunge wa Mwanakwerekwe, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba Mheshimiwa Rais anapokuwa madarakani kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hutekeleza majukumu yake mbalimbali kwa kuzingatia Ilani ya Uchaguzi ya Chama Tawala.

Ilani inatekelezwa katika kipindi cha miaka mitano na jukumu kuu la Serikali iliyoundwa na Chama Tawala ni kusimamia na kuhimiza malengo na mipango ya maendeleo. Kauli ya Rais kwa wananchi waliojipanga kujiletea maendeleo ni ahadi na huratibiwa na hatimaye kusambazwa katika Wizara zinazohusika kwa ajili ya utekelezaji.

Wizara husika kwa kushirikiana na Halmashauri huweka Makadirio ya utekelezaji wa ahadi mbalimbali katika Bajeti yake na zile za Halmashauri kulingana na uwezo wa Serikali au upatikanaji wa fedha. Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba pale ambapo utekelezaji wa mradi au mpango unaonyesha kuhitaji fedha nyingi zaidi huendelea kukamilishwa katika mwaka wa fedha unaofuata hadi utakapokamilika na kutoa huduma iliyotarajiwa.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya ahadi ni miradi mikubwa ya Maendeleo ambayo utekelezaji wake lazima utakuwa zaidi ya mwaka mmoja. Miradi kama hiyo ni ule wa Daraja la Mkapa kule Mto Rufiji, Uwanja wa Kisasa wa Mpira wa Miguu Jijini Dar es Salaam, Ukumbi wa Kisasa wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mjini Dodoma, Barabara kadhaa za Kitaifa za lami na kadhalika. Ni ukweli usiopingika kwamba baadhi ya miradi na ahadi za Serikali zimetekelezwa kwa zaidi ya muda uliotarajiwa kutokana na ufinyu wa Bajeti ya nchi yetu. Ili ahadi ziweze kutekelezwa kwa wakati, ni muhimu uchumi wa nchi yetu ukuzwe ili kuongeza pato la Taifa na hivyo kumudu utekelezwaji wa mipango na ahadi zote za Rais zilizoratibwa akiwa madarakani na kuweza kuendelezwa hata baada ya kipindi hicho kufikia ukomo yaani miaka mitano au kumi endapo atachaguliwa kwa vipindi viwili mfululizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahadi za Waheshimiwa Marais wa awamu zote zinatekelezeka. Baadhi zimetekelezwa na nyingine zinaendelea kutekelezwa kulingana na upatikanaji wa rasilimali. Wajibu wetu sisi Wabunge ni kuhamasisha wananchi ili kwa pamoja tufanye kazi kwa bidii, juhudi na maarifa, kwa lengo la kukuza pato letu na la Taifa. Hatua hiyo itaongeza uwezo wetu na kumudu kugharamia miradi na ahadi zote za Rais kwa faida na mafanikio ya wananchi wote.

**MHE. HAJI JUMA SEREWEJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kuniruhusu kuuliza swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri ninataka kuuliza swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa Chama cha Mapinduzi (CCM) ndicho kinachotawala na hii itaendelea milele mpaka mrudi. Na kwa kuwa yule Rais anayetawala kwa awamu nyingine baada ya kustaafu Rais aliyemtangulia wa Chama cha Mapinduzi.

Je, zile ahadi ambazo Rais aliyestaafu ameziweka kwenye majimbo Serikali haioni vizuri nazo kutekelezwa kwa huyo Rais ambaye ameshika madaraka yale ili kuzitekeleza vizuri zaidi ahadi zilizowekwa kwenye majimbo hayo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. DR. BATILDA S. BURIAN):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa kwamba ahadi za Rais zinatekelezwa hata baada ya Rais yule kuondoka madarakani.

Lakini hili linawezekana zaidi kama chama kile ambacho kilikuwa tawala kitaendelea kupewa ridhaa ya wananchi na kuendelea kupata ushindi. Tuna uhakika basi, ushindi wa Chama cha Mapinduzi ni ishara tosha kwamba ahadi za Marais wanaopita katika kila awamu zitaendelea kutekelezwa kila Rais yule atakapoondoka madarakani.

Naomba wananchi waendelee kuunga mkono Chama cha Mapinduzi ili tuweze kuendeleza kutekeleza ahadi hata Rais wetu anapomaliza muda wake. Nashukuru sana.

**MHE. ALI SAID SALIM:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja dogo la nyongeza.

Kama alivyojibu Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu kwamba hata Serikali ambayo inafuata utekelezaji kwa awamu ahadi hizo hutekelezwa. Nakumbuka katika kipindi cha Mheshimiwa Mkapa, Serikali iliweka ahadi kwamba itawalipa fidia walioathirika katika maandamano ya tarehe 26 na 27 Januari, 2001, lakini hadi hivi leo nazungumza ahadi hii bado haijatekelezwa. Je, hii ni ahadi kubwa nayo inahitaji muda mrefu na fedha nyingi, tunaomba kauli ya Serikali.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. DR. BATILDA S. BURIAN):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahadi ambayo inatolewa na Serikali makini muda wote inatekelezwa. Lakini napenda tu niseme kwamba ahadi iliyotolewa haikuwa ahadi ya kulipa fidia tulitoa ahadi kwamba tutatoa kifuta machozi na taratibu zinafanyika na ahadi hiyo itatekelezwa.

Na. 73

**Utengenezaji wa Daraja Kati ya Vijiji vya Kalole na Sandulula**

**MHE. ANNA R. LUPEMBE** aliuliza:-

Kwa kuwa, madaraja ni viungo muhimu kwenye barabara vinavyounganisha Kijiji na Kijiji kuwawezesha wananchi kusafiri na kuvuka kwenda eneo jingine kufanya shughuli zao:-

Je, Serikali ina mpango wa kutengeneza daraja linalounganisha vijiji vya Kalole na Sandulula?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Anna Richard Lupembe, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba madaraja ni moja ya viungo muhimu katika barabara ili kuwawezesha wananchi kuvuka kutoka eneo moja la barabara kwenda eneo jingine hususan inapokuwa barabara hiyo inakatisha eneo lenye bonde au mto wenye ukubwa unaohitaji daraja kuwekwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua umuhimu wa barabara katika Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga, kwa mwaka wa fedha 2007/08 Serikali imetenga kiasi cha shilingi milioni 417.15 kwa ajili ya matengenezo ya barabara. Fedha hizi ni kutoka Mfuko wa Barabara. Kati ya fedha hizo Halmashauri imetenga kiasi cha shilingi milioni 32.42 kwa ajili ya matengenezo ya madaraja na makalvati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kijiji cha Sandulula kipo katika barabara kuu ya Tunduma – Sumbawanga inayohudumiwa na *TANROAD.* Barabara hiyo inategemewa sana kwa ajili ya soko la mazao na huduma mbalimbali.

Aidha, kijiji cha Kalole kipo kati ya Kaengesa nacho pia kipo katika barabara Kuu ya Tunduma – Sumbawanga kwa upande wa pili ambayo ipo chini ya *TANROAD* na ndiyo inayotegemewa sana kwenda na kutoka maeneo ya masoko na huduma mbalimbali za kijamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Kalole-Sandulula inahitaji vivuko vya Madaraja ya *Culverts*. Katika mwaka huu wa fedha 2007/2008 kazi itakayofanyika ni ujenzi wa *culverts* kwa gharama ya shilingi 4,360,000/= zilizotengwa kwenye bajeti ya Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga. Kuhusu matengenezo ya daraja

linalounganisha vijiji vya Kalole na Sandalula alilozungumzia Mheshimiwa Mbunge, kwa mwaka huu wa fedha halijawekwa kwenye mpango wa matengenezo. Kwa kuwa vipaumbele kwa shughuli za maendeleo hupangwa na Halmashauri husika nashauri katika bajeti ya mwakani daraja hili liwekwe kwenye mipango ya Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga. Kama Wizara tutahakikisha kwamba daraja hilo limewekwa kwenye bajeti ya mwaka ujao kwa manufaa ya wananchi wa vijiji husika.

**MHE. ANNA R. LUPEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza naomba nikushukuru kwa majibu mazuri ambayo ameyajibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa wananchi wa Kalole wana mashamba yao ng'ambo ya Sandalula na ndiyo maisha yao wanalima huko na sasa hivi mvua zikinyesha hawawezi kwenda katika mashamba yao. Je, Serikali ina mikakati gani kwa dharura kwa kuwasaidia wananchi wa Kalole ili waweze kupata maisha yao bora kwa kila Mtanzania.

Vile vile kwa kuwa vijiji vingi nchini hapa vina matatizo kama hayo je, Serikali ina mikakati gani ya undani zaidi ili kuweza kuwasaidia wananchi kutatua matatizo yale?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERILI MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hatua za dharura nimeeleza kwamba kwa mwaka huu tutajenga kwanza ma-*culvert*, tukishajenga *culvert* ina maana kwamba baadaye tutajenga hilo daraja kama nilivyosema kwamba tutahakikisha kwamba mwaka ujao katika Bajeti tutaliweka hilo daraja kwa sababu kama mnavyofahamu kwamba Bajeti ya daraja mara nyingi inakuwa kubwa ukilinganisha na Bajeti za ma-*culvert*. Kwa hiyo, mwaka huu kama dharura tutahakikisha tumeweka *culvert* ili angalau wananchi hao waweze kuvuka kwenda kwenye mashamba yao.

Kwa mkakati wa ujumla Waheshimiwa Wabunge kama mlivyoona kwenye Bajeti ya Serikali ya mwaka huu kwamba fedha za barabara zimeongezwa na sisi kama Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) tumejipanga vizuri kuhakikisha kwamba fedha za barabara zilizokwenda kwenye Halmashauri zinatumika vizuri na zinajibu kero za wananchi hasa kwenye sehemu zile ambazo zina mahitaji makubwa, wananchi wanahitaji huduma hizo tutahakikisha kwamba barabara hizo zinatengenezwa kwa kiwango cha kupitika kwa mwaka mzima.

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, je Mheshimiwa Naibu Waziri anafahamu kwamba mimi ndio Mbunge wa jimbo hilo na kama hivyo ndivyo atakubaliana mimi kwamba kijiji cha Kalole hakiko katika Kata ya Kaengesa kiko katika Kata ya Sandulula na kwamba wala hakiko karibu na barabara ya Tunduma/Sumbawanga kiko mbali?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERILI MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimesema kwamba kijiji hicho kipo kandokando ya barabara inayokwenda Tunduma. Kwa hiyo, sio lazima kiwe barabarani, kinaweza kikawa pembeni mwa hiyo barabara ya Tunduma/Sumbawanga. Naomba

nikubaliane na Mheshimiwa Mbunge kwamba kuhusu Kata ni kweli kama alivyonisahihisha yeye mwenyewe. (*Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Hii nchi ni kubwa mpaka Waziri ajue Kata ni kazi kweli.

Na. 74

**Ujenzi wa Kiwanda cha Wanga – Chiwonga**

**MHE. JUMA A. NJWAYO (K.n.y. CAPT. GEORGE H. MKUCHIKA)** aliuliza**:-**

Kwa kuwa, Shirika la Maendeleo la Taifa *(NDC)* lilikuwa na mpango wa kujenga Kiwanda cha Wanga katika kijiji cha Chiwonga Wilayani Newala lakini mpaka sasa kiwanda hicho hakijajengwa:-

Je, ni nini kilisababisha kutojengwa kwa kiwanda hicho?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kapt. George Huruma Mkuchika, Mbunge wa Newala, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia lililokuwa Shirika la Viwanda vya Madawa *NCI* ilifanya uchunguzi juu ya uwezekano wa kuanzisha viwanda vya Wanga nchini mwaka 1979. Uchunguzi huo ulizingatia masuala mengi kama vile sehemu kunakopatikana muhogo kwa wingi, hali ya mawasiliano na miundombinu ya barabara katika eneo husika na upatikanaji wa maji, kwenye maeneo hayo na kadhalika.

Utafiti huo, ulibainisha kujengwa kwa viwanda vya Wanga vitatu kwa awamu katika maeneo ya Mikoa ya Mwanza, Tabora na Mtwara. Katika awamu ya kwanza Shirika lilijenga Kiwanda cha Wanga Sengerema mkoani Mwanza, hapo mwaka 1984. Awamu ya pili, ilihusu utafiti wa ujenzi wa Kiwanda cha pili ambapo kilikusudiwa kujengwa kijijini Nanda Wilayani Newala.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na hali mbaya ya uchumi katika miaka ya 1990, Shirika la Viwanda vya Madawa *NCI* lilishindwa kuendelea na hatua zaidi za mradi huo na ilipofika mwaka 1996, Serikali iliamua kufunga baadhi ya Mashirika yake likiwemo *NCI* na Miradi iliyokuwa chini yake ikahamishiwa Shirika la Maendeleo la Taifa *(NDC)* kwa utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa mradi huu haukuweza kutekelezwa kama ilivyokuwa imekusudiwa, napenda kumshauri Mheshimiwa Mbunge kwamba, kwa kuwa Wilaya ya Newala kwa ujumla ipo katika Ukanda wa Maendeleo wa Mtwara, (Mtwara *Development Corridor*) ambao utekelezaji wa miradi katika eneo hilo unaratibiwa na

*NDC;* bado kuna fursa ya kurejea azma iliyokuwepo awali ya mradi huu kwa wakati muafaka na kwa kushirikisha sekta binafsi. Natoa mwito kwa yeyote anayetaka ajitokeze kwa lengo la kuanzisha viwanda vya kutengeneza bidhaa mbalimbali kutokana na muhogo, popote nchini. *(Makofi)*

**MHE. JUMA A. NJWAYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri nina swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa nchi kama Nigeria imekuwa ikisafirisha sana muhogo mbichi kwenda kwenye nchi za Ulaya. Na kwa kuwa utaratibu huo una gharama nafuu sana. Jje, Serikali ina utaratibu gani wa kuanzisha utaratibu kama huu ili angalau wananchi wa Newala na maeneo mengine yanayolima muhogo waweze kunufaika?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana kabisa na Mheshimiwa Mbunge kwamba katika baadhi ya nchi ikiwemo na hiyo ya Nigeria wanao utaratibu wa kusafirisha muhogo kwenda nje kwa ajili ya kuuza.

Hapa nchini vile vile siku za nyuma tulikuwa na utaratibu ambapo muhogo kutoka Mkoa wa Mtwara na sehemu zingine nchini ilikuwa ikisafirishwa nje kwenda kuuzwa lakini baada ya kutetereka kwa vyama vya ushirika pamoja na utaratibu mzima tuliokuwa tunautumia hapo awali utaratibu ule ulisitishwa kidogo.

Lakini nataka tu nitoe mwito kwamba kwa sasa hivi Serikali bado inazingatia utaratibu wa kutafuta masoko ya mazao haya ikiwemo hilo la muhogo na kwa vile sasa hivi sera ya masoko inaandaliwa jambo kama hilo litazingatiwa. *(Makofi)*

**MHE. BENSON M. MPESYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa swali la msingi linazungumzia juu ya kujenga Kiwanda na moja kati ya ahadi za Rais ilikuwa ni kufufua viwanda katika maeneo ambavyo vilikuwa havifanyi kazi vikiwepo viwanda vya jiji la Mbeya. Nini mkakati wa Serikali kwa ujumla katika kuhakikisha viwanda ambavyo vilikuwa havifanyi kazi sasa vinafanya kazi kama utekelezaji wa ahadi ya Mheshimiwa Rais.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema katika kujibu swali la msingi kwamba utaratibu mzima wa kuanzisha viwanda sasa hivi kwa upande wa Serikali ni kuhakikisha kwamba inaweka mazingira muafaka ili kuleta vivutio kwa wawekezaji binafsi pamoja na watu wengine ambao wanaweza kujitolea ili kuanzisha viwanda hapa nchini hii ikiwa ni pamoja na kufufua viwanda ambavyo vilikuwa vinafanya kazi huko nyuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachotaka kusema hapa kwamba azma hiyo bado ipo na Serikali inaendelea na hatua zake mbalimbali za kuhakikisha kwamba inaweka mazingira muafaka ili kuvutia wawekezaji ili kuweza kufufua viwanda.

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba kazi ya kubinafsisha viwanda ni kama imefikia mwisho. Lakini kuna baadhi ya miji ambayo viwanda vyake bado hata ule ubinafsishaji wenyewe umekuwa haijafanyika vizuri. Walipatikana wawekezaji lakini hawakuanzisha hivyo viwanda mojawapo ni Moshi na Mbeya.

Kuhusu Mbeya swali la Mheshimiwa Mbunge ni kwamba unafanyika utafiti sasa hivi Kitaifa kutambua tatizo limetokea wapi. Kwa mfano kule Mbeya kuna Kiwanda cha Zana za Kilimo ambacho kilikuwa kinatengeneza majembe ya mkono lakini kwa muda mrefu sasa hakitengenezi na hawapatikani watu wanaotaka kutengeneza majembe ya mkono. Kwa hiyo, lazima tujiulize.

Je, tuendelee na majembe ya mkono ama tutengeneze aina nyingine ya zana za kilimo na kazi hiyo inafanyika.

Kwa hiyo, ningependa kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba chini ya utaratibu wa Kamati inayofanya kazi chini ya Mheshimiwa Waziri Mkuu utafiti huo unaendelea na baadaye Serikali itatathmini na kuamua nini kifanywe kwa vile viwanda ambavyo bado havijapata mwekezaji au vimepata mwekezaji lakini havizalishi.

Na. 75

**Kuwepo Kwa Mlango wa Dharura Kwenye Magari ya Abiria**

**MHE. JOYCE M. MASUNGA (K.n.y. MHE. RUTH B. MSAFIRI**) aliuliza:-

Kwa kuwa, kigezo kimojawapo muhimu cha basi kuruhusiwa kubeba abiria ni pamoja na kuwa na mlango wa dharura, na vioo vinavyofunguka kwa haraka pindi shida inapotokea; na kwa kuwa, imethibitika kuwa, magari mengi ya abiria licha ya kuwa ni Malori, yaliyojengewa bodi za mabasi lakini hayana milango ya dharura, hali inayoongeza idadi ya majeruhi na vifo pindi ajali mbaya zinapotokea:-

(a) Je, Serikali imejiandaa vipi kuhakikisha kuwa magari yote ya abiria yanakuwa na milango ya dharura na madirisha yanayofunguka kwa haraka;

(b) Je, Serikali inadhibiti vipi malori yanayojengewa bodi ili yatumike kwa usafiri wa abiria;

(c) Je, kuna muda wowote maalum uliowekwa wa kutekeleza hayo yaliyoelezwa kwenye sehemu ya (a) na (b) ya swali hili?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Usalama wa Raia, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Ruth Blasio Msafiri, Mbunge wa Muleba Kaskazini, lenye sehemu (a), (b) na (c), napenda kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba vigezo vinavyokubalika ili basi liruhusiwe kubeba abiria ni pamoja na kuwa na milango ya dharura na madirisha yanayofunguka kwa urahisi, matairi bora na imara, bodi iliyotengenezwa katika ubora unaokubalika na dereva mzuri anayezifahamu Sheria za Usalama Barabarani.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, kwa niaba ya Mheshimmiwa Waziri wa Usalama wa Raia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ruth Blasio Msafiri, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja na kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Jeshi la Polisi, *SUMATRA* na *TBS* tarehe 2 Novemba, 2007 imetoa tamko rasmi kwamba mpaka kufikia tarehe 1 Mei, 2008 mabasi yote ya abiria lazima yawe na milango ya dharura au madirisha maalum yanayofunguka kwa urahisi, na mabasi yote ambayo bodi zake zimejengwa kwa kutumia *chassis* za malori yawe yamefanyiwa marekebisho.

Aidha, ujenzi wa bodi zote za mabasi lazima uzingatie kiwango cha *TBS* cha bodi za mabasi Na. 598.1999 kwa mujibu wa Sheria Na. 3 ya mwaka 1975 ya *TBS* ambayo inaelekeza kwamba bodi za mabasi zijengwe katika *chassis* zenye injini maalum za mabasi na zenye milango ya dharura.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya tamko hilo la Serikali la tarehe 2 Novemba, 2007 *SUMATRA* haitasajili basi lolote la abiria ambalo halitakuwa limekidhi kiwango Na. *TBS. 598.1999.*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukaguzi wa mabasi yaendayo mikoani unaonyesha kwamba karibu asilimia 50 ya mabasi yamejengwa katika *chassis* za malori.

Hivyo bila kuathiri shughuli za kijamii na kiuchumi za wananchi wetu, Serikali imetoa miezi sita kwa wamiliki wote wa mabasi hapa nchini kuyafanyia marekebisho mabasi yenye *chassis* za malori na yasiyo na milango rasmi ya dharura kufanya hivyo kabla ya tarehe 1 Mei, 2008. Mabasi yasiyokidhi kiwango cha *TBS Na. 598.1999* hayataruhusiwa tena kusafirisha abiria hapa nchini. *(Makofi)*

**MHE. LUCY T. MAYENGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwa kuwa Serikali wale watu wote waliohusika na kuweza kufuatilia viwango vinavyoruhusu mabasi kutembea barabarani bado wapo na mabasi haya ambayo yana- *chassis* za malori yalikuwa bado yapo barabarani. Je Serikali haioni umuhimu wa sasa kuchukua hatua kwa wale watu wote ambao wamehusika kwa sababu malori haya yameua watu wengi sana?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema katika jibu langu la msingi kwamba Serikali imetoa muda maalum ambayo hayatimizi vigezo. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na wananchi kwamba Jeshi la Polisi litasimamia utaratibu huo ili kuhakikisha mabasi yote yale ambayo hayatimizi vigezo hivyo hayatatembea barabarani.

Na. 76

**Madai ya Askari Polisi**

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA (K.n.y. MHE. SHOKA KHAMIS JUMA)** aliuliza:-

Kwa kuwa, Askari Polisi wanadai malimbikizo ya fedha zao kwa muda mrefu sasa na kwa kuwa mwaka wa fedha 2006/2007 walilipwa lakini malimbikizo hayo hayakumalizika:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuondoa kero hiyo ya kudaiwa na Askari?

**NAIBU WA USALAMA WA RAIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Usalama wa Raia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, Mbunge wa Micheweni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli pamoja na juhudi za Serikali kupunguza madeni yanayotokana na stahili mbalimbali za Askari Polisi bado Jeshi la Polisi linaendelea kuwa na madeni yatokanayo na stahili hizo. Hii inatokana na uasili wa kazi za Jeshi la Polisi ya kulinda usalama wa raia na mali zao.

Kuna matukio ambayo ni muhimu na lazima yatekelezwe kwa wakati bila kujali uwepo wa fedha. Hali hii husababisha kuongeza malimbikizo ya madeni ya stahili zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2006/2007 Serikali ilitenga jumla ya shilingi bilioni 8.5 mpaka Juni, 2005. Kati ya madeni hayo madeni yaliyohakikiwa ya jumla ya shilingi bilioni 5.4 yameshalipwa. Serikali itaendelea kushughulikia madeni yaliyosalia kipindi hicho pamoja na madeni mapya yaliyojitokeza kati ya kipindi cha Julai, 2005 mpaka Juni 2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii kuwapongeza Askari Polisi kwa kufanya kazi ya kuhudumia wananchi katika mazingira magumu.

Pamoja na hali hiyo, Serikali inaendelea na jitihada za kutafuta ufumbuzi wa suala hili kwa kuboresha Bajeti ya Jeshi la Polisi kutoa uhamisho kwa Askari Polisi pale tu inakupokuwa lazima kufanya hivyo, Askari kulipwa stahili zao kabla ya kwenda likizo, kuwalipa Askari Polisi kabla ya kuanza safari zao za kikazi pamoja na kuanzisha

mpango wa maboresho katika Jeshi la Polisi ili kupunguza matatizo yanayowakabili likiwemo suala la malimbikizo ya madeni. Ninaimani mpango huu wa maboresho utakuwa suluhisho la matatizo hayo.

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi nakushukuru ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri ninapenda kumwuliza kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa miongoni mwa malimbikizo ambayo yanawasumbua sana Askari Polisi na familia zao ni ya wale waliofariki dunia ikawa hawajalipwa warithi wao. Sasa Je Serikali haioni kuwa angalau hili linapaswa kuharakishwa haraka ili na wale warithi wasije wakafariki ikabidi kutafuta mtandao mwingine wa warithi?

Malimbikizo yanayowasumbua pia Askari ni yale ya chakula pamoja na malimbikizo ya uhamisho. Kwa kuwa hawa Askari ni watu wenye kufanya majukumu muhimu kwa taifa letu. Je, Serikali haioni inafaa kutoa kipaumbele angalau kwa hili, ili kuwafanya Askari wetu ikawa motisha wa kufanya kazi nzuri?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Khalifa kwamba upo umuhimu wa wale Askari ambao wamefariki dunia kupewa upendeleo maalum kwa ajili ya malipo yao na hatua hizo zimechukuliwa ndani ya Jeshi la Polisi. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na wananchi kwamba kazi ya malipo hayo inaendelea vizuri na muda usio mrefu hali hiyo itakuwa imerekebishwa.

Kuhusu swali la pili, malimbikizo ya chakula na uhamisho. Kama nilivyosema katika jibu langu la msingi kwamba sasa kuhusiana na suala la uhamisho litatoka kwa dharura maalum kwa kuondoa usumbufu huu ambao wakati mwingine Askari wanaupata. Lakini tunachukua kila hatua kuhakikisha kwamba Askari wetu wanaondokana na tatizo hili la malimbikizo ya madeni. Tunafanya kila jitihada tatizo hili liondoke ili askari wetu waweze kutoa huduma nzuri kwa wananchi.

**MHE. MARTHA M. MLATA**: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Mimi napenda kumwuliza Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba katika majibu yake amesema stahili hizo huwa zinashindwa kutekelezwa kutona na dharura ambazo zinajitokeza. Sasa je, haoni kwamba Wizara yake ina umuhimu wa kutenga fungu la dharura ili kutokugusa stahili za Askari hawa na kuwaacha waweze kufanya kazi zao bila matatizo? Ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu inaona umuhimu wa kuweka fungu la dharura hilo lipo. Lakini tatizo lililopo ni udogo wa Bajeti yenyewe, kutokana na hali halisi ya uchumi wa nchi yetu. Mara hali itakapokuwa nzuri na tukawa na fedha za kutosha katika Bajeti tatizo hilo litaondoka. *(Makofi)*

Na. 77

## Ujenzi wa Kituo cha Uhamiaji – Muhukuru

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA** aliuliza:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya sijamwomba Mheshimiwa Naibu Waziri ajibu swali langu namba 77 ninapenda kuchukua nafasi hii kuwapa pole sana wananchi wa Jimbo la Peramiho na Halmashauri nzima ya Wilaya ya Songea, kwa kufiwa na Diwani wetu mpenzi ambaye amefariki jana tarehe 5 Novemba, 2007 Mtegeta na sasa hivi tunaendelea kuwasiliana kuona ni namna gani tunamzika Diwani huyo kwa heshima na taadhima kubwa katika Halmashauri yetu katika Kata anayotoka. Baada ya kuyasema hayo ninaomba sasa swali langu Namba 77 liweze kujibiwa.

Kwa kuwa katika kupitisha Bajeti ya Wizara ya mwaka 2007/2008, Serikali ilithibitisha Bungeni kuwa itatimiza ahadi yake ya kutumia shilingi milioni ishirini (20,000,000/=) kujenga kituo cha Uhamiaji eneo la Kata ya Muhukuru, Songea Vijijini, mahali ambapo panajengwa Daraja la Umoja Na.2:-

(a) Je, mpaka sasa fedha hiyo imeshaidhinishwa?

(b) Kama bado ni lini Serikali itafanya hivyo?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jenista Joachim Mhagama, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoeleza katika hotuba yangu ya Bajeti, niliyowasilisha katika Bunge la ko Tukufu, tarehe 31 Julai, 2007 ujenzi wa Ofisi ya Uhamiaji katika Kituo cha Muhukuru utatekelezwa katika mwaka wa fedha 2007/2008.

Mheshimiwa Naibu Spika, kiasi cha fedha zilizotajwa katika Bajeti zimekwisha idhinishwa na zimepelekwa kwa Afisa Uhamiaji Mkoa wa Ruvuma kwa *warrant of funds* No. 00236437 ya tarehe 17/10/2007 kwa ajili ya ujenzi huo.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa ujenzi wa daraja kule sasa umeshakamilika na kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri ameshatoa taarifa rasmi kupelekwa kwa fedha hiyo kwa ajili ya kupelekwa kwa fedha hiyo kwa ajili ya kujenga Kituoa cha Uhamiaji. Lakini kwa kuwa sababu nyingine iko kubwa ya umaana wa uhamiaji na usalama wa raia kwa maana ya kituo cha polisi ni kama watoto mapacha waliozaliwa kwa mama mmoja, lakini matumbo tofauti. *(Makofi)*

Je, Mheshimiwi Naibu Waziri haoni sasa ni wakati muafaka wa kushirikiana kati ya Wizara husika na Wizara yake ili kujenga na Kituo cha Polisi sambamba na Kituo hicho cha Uhamiaji kwa ajili maendeleo ya wananchi hapo mpakani na wale jirani zetu wa Msumbiji?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana naye kwamba Wizara yetu ya Usalama wa Raia na Wizara ya Mambo ya Ndani ni kama watoto mapacha na tunafanya kazi kwa pamoja na ndiyo maana nipo hapa kujibu swali kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri. Upo mpango wa kujenga kituo cha polisi katika eneo lile na Mheshimiwa Mbunge anajua, mara fedha zitakapopatikana kazi hiyo itaanza mara moja.

Na. 78

**Hitaji la Umeme – Muheza**

**MHE. HERBERT J. MNTANGI** aliuliza:-

Kwa kuwa Mji mdogo wa Muheza ndio Makao Makuu ya Wilaya ya Muheza ambao unakua kwa kasi kubwa kwa ujenzi wa nyumba za kisasa katika mitaa ya Michungwani, Masuguru/Masimbani, Genge, Mdote na Mbaramo/Kisiwani na kwa kuwa kwa muda mrefu sasa *TANESCO* imekosa uwezo wa kusambaza umeme katika maeneo hayo ya mji mdogo wa Muheza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuisadia *TANESCO* kusambaza umeme katika maeneo hayo ya Mji mdogo wa Muheza?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge Herbert Mntangi, Mbunge wa Muheza ninapenda na mimi nitumie nafasi hii kukipongeza sana Chama cha Mapinduzi kwa uchaguzi ambao umekamilika jana. Lakini pia niwapongeze sana wajumbe ambao waliwapigia kura wagombea nikiwemo mimi na niwatie matumaini kwa wale ambao kura zetu hazikutosha. Tunampongeza sana Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri Mkuu na viongozi wetu kwa kupata ushindi wa kishindo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema maneno hayo ya utangulizi sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mbunge wa Muheza, kama ifautavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli maeneo mengi katika Mji wa Muheza yanakuwa kwa kasi na hivyo kuhitaji nishati ya umeme kama kichocheo na nyenzo muhimu katika kufanikisha maendeleo ya wananchi wa mji huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mitaa iliyotajwa na Mheshimiwa Mbunge ya Michungwani, Masuguru/Msimbazi, Genge, Mdote na Mbaramo/Kisiwani tayari ina umeme muda mrefu ila kilichobaki ni upanuzi na ujenzi wa mifumo ya usambazaji umeme ili kufanikisha lengo la kuwapatia huduma ya umeme wateja wapya.

Serikali ina nia ya kusambaza umeme katika maeneo hayo pamoja na maeneo mengine. Kikwazo kikubwa katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya umeme imekuwa ni ukosefu wa fedha za kutosha kutekeleza miradi hiyo. Hata hivyo, Serikali imekuwa ikifanya juhudi za kutafuta fedha kutoka vyanzo vya ndani na nje ya nchi ili kutekeleza miradi ya kusambaza umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Muheza kwa juhudi za Serikali za kutafuta fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya kusambaza umeme katika maeneo mengi Wilayani Muheza imezaa matunda na mji mdogo wa Muheza umejumuishwa kwenye miradi ambayo iko chini ya ufadhili wa Serikali ya Marekani kupitia mpango wa *Millenium Challenge Corporation (MCC).* Tunamwomba Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Muheza waendelee kuvuta subira wakati maandalizi ya utekelezaji wa mpango huo yakiendelea.

**MHE. HERBERT MNTANGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri aliyotoa hata hivyo naomba nimwulizwe swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa tatazo la ukosefu wa fedha hasa kwa *TANESCO* hasa katika utekelezaji wa shughuli zake umechangia kwa kiasi kikubwa kushindwa kutelezwa kwa ahadi za Wizara hii ya Nishati na Madini katika maeneo mengi hapa nchini.

Je, Wizara ina utaratibu gani kuhakikisha kwamba *TANESCO* inaratibu ahadi zote za Wizara ya Nishati na Madini na kutengeneza Mkakati wa kuhakikisha kwamba ahadi hizo zinatekelezwa?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, *TANESCO* ina mipango mingi mizuri na ahadi nyingi zilizopo sasa hivi zilizowahi kutolewa na Wizara zinaratibiwa na zinafahamika. Kikwazo ambacho kimekuwa kikikwamisha kasi ya utekelezaji wa miradi hii ambayo mingi ilisharatibiwa na ikafanyiwa tathimini kwa kweli ni upungufu wa fedha. Hili ndiyo tatizo kubwa ambalo limekuwa likituchelewesha na kwa tafsiri nyingine inaweza ikaonekana kama vile uratibu wake unakuwa hauendi kama ambavyo wananchi wanatarajia.

Lakini ukweli ni kwamba *TANESCO* na Serikali vinaratibu vizuri mipango yake na ahadi ambazo zimetolewa lakini tunazidi kuwaomba wananchi kwamba waelewe Serikali iko makini kwa ufuatiliaji katika kutekeleza hizo ahadi hasa baada ya upatikanaji wa fedha kuwa mzuri.

Na. 79

**Madini Kutokuwa Suala la Muungano**

**MHE. ALI SAID SALIM** aliuliza:-

Kwa kuwa wakati Serikali ilipokuwa ikijibu swali kupitia Wizara ya Nishati na Madini, katika Mkutano wa Bajeti mwaka 2007 ilisema madini si jambo la Muungano, ila mafuta na gesi ndiyo ya Muungano

Je, Serikali haioni kuwa hiyo ni kasoro hasa ikizingatiwa kuwa mambo hayo yako Wizara moja?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ali Said Salim, Mbunge wa Ziwani, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, inaeleza bayana kuwa suala la mafuta na gesi ni miongoni mwa mambo ya Muungano, bali madini siyo suala la Muungano.

Kwa kuzingatia Katiba ya Jamhuri ya Muungano ambayo ndiyo inayotoa mwongozo wa Sheria zote za nchi Wizara haioni kuwepo kwa kasoro yoyote kwa madini kutokuwa jambo la Muungano wakati mafuta na gesi ni ya Muungano licha ya mambo yote hayo kushughulikiwa na Wizara moja. Pamoja na kuwa kwa sasa maliasili madini si ya Muungano, lakini mapato yanayotokana na madini yanakwenda moja kwa moja kwenye mfuko mkuu wa mapato ya Serikali ambao ndiyo unaogharamia uendeshaji wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano.

**MHE. ALI SAID SALIM:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa majibu hayo ambayo binafsi sikuridhika nayo Serikali. Hata hivyo nina maswali mawili ya nyongeza. La kwanza, kwa kuwa ratiba si msaafu. Je, haionekani sasa kwamba katika kuimarisha Muungano wetu ni vyema na madini nayo yakawa ni suala la Muungano? Swali la pili, Je, hivi sasa kwa mawazo yangu mimi mafuta yamefanywa ni suala la Muungano kwa sababu kuna fununu kwamba yapo Zanzibar. Leo mungu akifanya rehema zake Zanzibar kukawa na dhahabu, hamtafanya kuwa ya Muungano?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri ni kwamba kwa sasa hivi katiba iko wazi, mafuta ni suala la muungano. Madini siyo suala Muungano. Lakini hata Mheshimiwa Mbunge kama angekuwa anapenda madini yaingie kwenye vipengele vya Muungano, tuna utaratibu ndani ya Katiba ni nanma gani ya kuongeza vipengele katika Katiba yetu. Imewahi kufanyika. Kwa utaratibu huo ikionekana inahitajiwa taratibu zitafuatwa. Lakini kwa sasa hivi madini si suala la Mungano na kama alivyoeleza, fedha za madini zinaingia kwenye mfuko mkuu ambao ni wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambao unaendesha Muungano. Kwa hiyo, kwa namna hiyo unaweza kusema kwamba ile pesa inayopatikana kutoka kwenye madini vilevile inatumika katika kuhudumia masuala ya Muungano. *(Makofi)*

Lile la kusema kwamba kwa sababu Zanzibar kuna mafuta. Tuna kampuni zaidi 11 ambazo zina leseni za utafutaji wa mafuta; na kampuni zilizo nyingi karibu zote ziko

katika mwambao mwa Tanzania Bara na kule majini pamoja na nchi kavu. Vile vile kuna vitalu vipo katika maeneo ya Zanzibar. Kwa hiyo, huwezi ukajua mafuta yatapatikana wapi. Yanaweza kupata mahali popote hapa nchini lakini yakipatikana itakuwa ni rasilimali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Na 80

**Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi**

**MHE. MBARUK KASSIM MWANDORO** aliuliza:-

Kwa kuwa wananchi wamehamasika sana kuhusu Sera za Uwezeshaji Kiuchumi ili hatimaye kila Mtanzania aishi maisha bora, na kwa kuwa, wananchi wamekuwa wakikwamishwa na vikwazo vingi katika utekelezaji wa miradi mbalimbali nchini kama vile *TASAF* na kadhalika:-

(a) Je, Serikali inachukua hatua gani kupambana na urasimu na ukwamishaji wananchi kinyume cha matarajio?

(b) Je, Serikali haioni umuhimu wa utekelezaji wa miradi hiyo ya maendeleo kuambatana na vigezo muhimu katika kutathmini utendaji wa Watendaji wa ngazi mbailmbail na hivyo kutumia utaratibu wa *OPRAS* kwa makini zaidi?

(c) Je, si vema kwa Serikali kuwachukulia hatua kali za kinidhamu Watendaji ambao wanazembea katika kufanikisha programu zinazokusudia kuwasaidia wananchi?

**NAIBU WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI** alijibu:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali katika suala zima la kuondoa vikwazo vinavyoweza kukwamisha wananchi katika utekelezaji wa miradi mbalimbali nchini. Mojawapo ya hatua hizi ni kuweka taratibu mbalimbali zinazozingatia uwazi na uwajibikaji katika kutekeleza miradi husika ili hatimaye kila Mtanzania aishi maisha bora.

Kwa mfano, utaratibu uliowekwa na mradi wa *TASAF* awamu ya pili unahitaji kwamba, kabla ya miradi iliyoibuliwa na wananchi kupatiwa fedha makabrasha yote yanayopokelewa Makao makuu ni lazima yapatiwe na maafisa miradi waliopo *TASAF* Makao Makuu kuhakikisha kwamba vigezo vyote vya kupata fedha toka *TASAF* vimetimizwa na nyaraka zote zinazohitajika zimeambatanishwa. Baada ya hapo, utaratibu unataka miradi hiyo ipelekwe kwa watalaamu wa Sekta husika ili nao waangalie kama viwango vya Sekta husika vimezingatiwa kabla hawajapendekeza miradi hiyo ipelekwe kwenye Kamati ya Uongozi ngazi ya Taifa inayosimamia mradi (*National Steering Committee*) kuruhusu malipo yafanyike ili mradi husika uweze kutekelezwa.

Hivyo basi, ucheleweshaji unaweza kutokea kama matayarisho ya makabrasha yanayopokelewa *TASASF* Makao Makuu yanakuwa yahajakamilika. Hii husababisha muda mwingi kupotea hasa pale inapobidi kufanya mawasiliano na Waratibu ili kasoro hizo zirekebishwe. Jinsi waratibu wa Halmashauri wanavyowasilisha nyaraka kamili au wanavyorekebisha mapungufu mapema, ndivyo fedha za miradi zinavyotolewa mapema. Hakuna ukwamishaji wowote unaofanywa zaidi ya kuzitaka jamii kuzingatia taratibu zilizowekwa. Kwa maana ya utekelezaji mzuri wa miradi nchini. Mradi wa *TASAF* umeonyesha mafanikio makubwa na hauwezi kutumika kama mfano wa ukwamishaji wananchi.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaona umuhimu na inaafiki kabisa kwamba utekelezaji wa miradi ya maendeleo ukiambatana na vigezo muhimu katika kutathmini utendaji wa Watendaji kwa ngazi mbalimbali utaboresha zaidi faida zitokanazo na miradi hiyo. Hivyo, upimaji wa utendaji kazi kwa watuimshi wa umma kwa njia ya wazi au *OPRAS* ni mojawapo ya njia ambazo zinaweza kuleta ufanisi zaidi katika utekelezaji wa miradi husika.

Mradi wa *TASAF* awamu ya pili unatumia pia mbinu shirikishi za jamii (*Community Score Card*) katika kufuatilia na kutathmini Miradi ikiwemo kupima ufanisi na uwajibikaji wa Watendaji katika ngazi mbalimbali. Utaratibu huu unahusisha wananchi kupima ufanisi wa Watendaji kwa kutumia viashiria mbalimbali na baadaye kufanya mkutano wa majumuisho kati ya mtoa huduma yaani mtendaji na anayaepokea huduma, yaani mwananchi kuweza kuzungumza na kuweka bayana mafanikio na vikwazo ambavyo vinaweza kuathiri ufanisi. Hivyo kwa kutumia utaratibu huu kunawezesha wahusika kuweka mipango ya pamoja na kuhakikisha kuwa matatizo yailiyojitokeza yanatatuliwa na Watendaji wanaotoa huduma ipasavyo.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuwa daima ikiwachukulia hatua za nidhamu Watendaji waliobainika kuzembea katika kufanikisha programu ikiwa ni pamoja na kusitisha au kutokuendeleza mikataba ya Watendaji hao.

**MHE. MBARUK KASSIM MWANDORO:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri napenda kuuliza swali moja la nyongeza kama ifuatavyo:-

Katika utekelezaji wa miradi hiyo pamekuwepo na ucheleweshaji na sababu zimeelezwa. Lakini napenda nielewe iwapo Serikali imechukua hatua gani thabiti kufuatilia kiuthabiti na kubaini dosari na vikwazo vilivyoko na hatua gani thabiti ili mambo hayo yasikwame?

**NAIBU WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua kwamba katika kuanzisha programu au miradi yoyote ile patakuwepo na matatizo mbalimbali yakiutendaji na ya kiutekelezaji na Serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali za kurekebisha kasoro zinazojitokeza

ikiwa ni pamoja na kuwachukulia hatua watendaji wanaohusika, aidha hatua za kinidhamu au vinginevyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili linaratibiwa zaidi na Halmashauri zetu za Wilaya na watendaji wote wanaoratibu miradi ya *TASAF* ni watendaji ambao wapo chini ya himaya za Halmashauri za Wilaya ambapo sisi Waheshimiwa Wabunge tunatoka. Kwa hiyo, natoa wito kwamba tushiriki kikamilifu katika kufuatilia miradi hii na utendaji wa hao wafanyakazi wa Halmashauri ili kasoro zinapojitokeza tusaidiane katika kuchukua hatua zinazotakiwa.

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza. Kwa kuwa katika Wilaya ya Kahama kuna miradi mingi ya ujenzi wa nyumba za Walimu na vyumba vya madarasa ambazo wananchi walianza kujenga muda mrefu kabla ya *TASAF* awamu ya pili. Baada ya *TASAF* kuwa wamekuja wameomba wananchi hao kwamba miradi yao iingizwe katika mpango wa *TASAF* na thamani ya majengo yenyewe yanazidi asilimia 20 ambayo *TASAF* wanasema wananchi wachangie lakini *TASAF* wamekuwa wakikataa kuingiza miradi hii wakisema kwamba wananchi waanze miradi mipya ndiyo itakayoingizwa.

Je, Serikali haioni kwamba huu ni moja ya ukwamishaji ambao Mheshimiwa Mbunge amezungumzia na hivyo unapaswa uondolewe ili miradi hii ikamilishwe kwa sababu tayari wananchi wameshachangia?

**NAIBU WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, swali ambalo Mheshimiwa Mbunge ameliuliza ni swali *specific* ni *case* peke yake ningependa kumwomba Mheshimiwa Mbunge atuletee hii kesi ofisini ili tuweze kuona ni wapi ambapo ukwamishaji unatokea. *(Makofi)*

Na. 81

**Kazi za *TASAF***

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE** aliuliza:-

Kwa kuwa *TASAF* ni chombo cha Serikali; na kwa kuwa fedha nyingi za Serikali zinapitia katika chombo hicho.

Je, Serikali itakubaliana nami kuwa chombo hicho kikiundwa kisheria kitakuwa endelevu katika kusukuma Maendeleo katika ngazi ya jamii (*An Agency for Community Development in Tanzania)?*

**NAIBU WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI** alijibu**:-**

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa, kama ifuatavyo:-

Kimsingi ninakubaliana na mapendekezo ya Mheshimiwa Mbunge. Tangu *TASAF* ilipoanzishwa kumekuwepo na ongezeko la miradi ya fedha ambazo zimekuwa zikipitishwa katika chombo hiki. Wakati wa awamu ya kwanza katika kipindi cha mwaka 2000 – 2004 miradi iliyotekelezwa kwenye Wilaya 40 Tanzania Bara na Visiwani ni 1,704 kwa Bajeti ya Dola za Kimarekani milioni 73.

Hii ikijumuisha michango ya Serikali, mikopo kutoka Benki ya Dunia na Jamii. Katika awamu ya pili ya *TASAF* inayotekelezwa katika nchi nzima kwa miaka mitano kuanzia mwaka 2005 – 2009 miradi 5,950 inatarajiwa kutekelezwa kwa Bajeti ya Dola za Kimarekani milioni 178. *(Makofi)*

Hadi kufikia mwisho wa Septemba 2007, jumla ya miradi 2,582 ilitekelezwa na jamii chini ya usimamizi wa *TASAF* na Halmashauri husika. Tunazo pia fedha za wadau wengine zinazopitishwa *TASAF* kwa ajili ya miradi katika ngazi za jamii kiasi cha Dola milioni 24. Wadau hao ni pamoja *Marine and Coastal Environmental Management Project (MACEMP), Zanzibar Aids Commission (ZAC)* na *Training and Participation (TRP)*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na majukumu muhimu ya kuondoa umaskini yanayotekelezwa na Mfuko wa *TASAF*, Serikali tayari imeliona suala linalopendekezwa na Mheshimiwa Mbunge na hivyo uanzishwaji wa *TASAF* kisheria ni miongoni mwa masuala yatakayojadiliwa wakati wa mapitio ya kati ya *TASAF II* mwezi Novemba 2007 hadi Februari 2008.

Ningependa kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa Serikali na wadau wengine watalijadili suala hili na hatimaye kupata muafaka juu ya namna bora zaidi ya kuendeleza mazuri yaliyotokana na kuanzishwa kwa *TASAF* kwa faida ya jamii na maendeleo ya nchi yetu kwa ujumla. Uundwaji wa chombo hiki kisheria ni moja ya masuala yatakayojadiliwa. *(Makofi)*

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Naibu Spika nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa chombo hiki ni muhimu sana katika Maendeleo ya nchi yetu na kwa kuwa katika Bajeti ya 2007/2008 fedha zilizotengwa kwa ajili ya Miradi ya *TASAF* ni bilioni 55 fedha za nje na bilioni 3 fedha za ndani. *(Makofi)*

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri atakubaliana nami kwamba ili chombo hiki kiwe endelevu iko haja kwa fedha za ndani kuongezwa badala ya kutegemea zaidi hizi fedha za nje?

**NAIBU WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Lubeleje kwa

kufuatilia masuala mbalimbali muhimu ya Kitaifa na hususan yale ya Jimbo lake. Mheshimiwa Lubeleje, pongezi nyingi sana! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana naye kabisa kwamba bajeti yote ya fedha za ndani katika mradi huu ni ndogo na iko haja kubwa ya kuweza kuongeza uwezo wetu wa ndani ili ikiwezekana mradi huu wa *TASAF* utumie fedha za ndani. Lakini kama mnavyoelewa, tatizo ni uwezo wetu wa ndani kuweza kufikia kiwango hicho. Serikali ya Awamu ya Nne, imeweza kuongeza kwa kiwango kidogo. Ni matarajio yetu kwamba tutaendelea kuongeza wigo wa kodi ili tuweze kupata fedha za ndani kukidhi mahitaji yote ya *TASAF II.*

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, *TASAF* kinadharia inaonekena kama haina urasimu lakini unapokwenda kwenye utekelezaji, kwa kweli ugoigoi ni mkubwa mno. Sijui Serikali inataka kusema nini juu ya hali hii ambayo Wabunge karibu wote tunakutana nayo na kwamba mradi wa *TASAF* ili ukamilike unachukua karibu miaka miwili au zaidi kutoka hatua ya kwanza?

Je, Serikali haioni kwamba kuna sababu ya kufanya marekebisho ya miradi ya *TASAF* ili kuondoa urasimu na huu ugoigoi ili uweze kutekelezeka kwa muda mfupi? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, sikubaliani naye kwamba miradi ya *TASAF* kuna ugoigoi mkubwa kiutekelezaji lakini kinadharia inaonekana ni mizuri. Sikubaliani naye kabisa kwa sababu ninazo takwimu za kuthibitisha hilo. Kwa mfano, *TASAF II* bajeti yake inatakiwa kutekeleza miradi 5,950 katika kipindi cha uhai wake yenye jumla ya thamani ya *U$* Milioni 178 lakini mpaka kufikia mwezi Septemba ilikuwa imeshatekeleza miradi 2581, karibu nusu ya miradi yote inayotakiwa kuitekelezwa ambayo tayari lengo lake kiutekelezaji liko katika njia. Kwa hiyo, huwezi kwa namna yoyote ile kusema kwamba kuna ugoigoi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naweza kukubaliana naye kwamba kuna *cases* mbalimbali katika Halmashauri mbalimbali na miradi tofauti tofauti ambapo ucheleweshaji upo. Lakini, kama nilivyosema katika jibu langu la msingi kwamba wale watendaji wa *TASAF* wako chini ya Halmashauri za Wilaya ambako na sisi Waheshimiwa Wabunge tunatoka huko.

Kwa hiyo, napenda sana na ningefurahi kuwakaribisha Waheshimiwa Wabunge katika Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, wafike tujadili pale wanapoona kuna matatizo yanayohusu *TASAF* na tutajadiliana na kuwaita viongozi wa *TASAF* wanaohusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini, pili, nimesema katika jibu langu la msingi kwamba sasa hivi mazungumzo yataanza namna ya kuweza kuiboresha *TASAF II* katika kipindi hiki cha mwezi Novemba mpaka Januari mwaka kesho. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Labda uitishe semina hapa hapa, wamhoji huyo mtu! *(Makofi/Kicheko)*

Na. 82

**Hitaji la Mafundi Mchundo Nchini**

**MHE. JANET B. KAHAMA** aliuliza:-

Kwa kuwa vifaa vinavyotumika hospitalini katika upimaji na utafiti kama *X-Ray, Ultra-Sound, MRI Machines, CT-Scan* na kadhalika huharibika mara kwa mara katika Hospitali nyingi za Rufaa nchini; na kwa kuwa Mafundi Mchundo *(Technicians)* ni haba hali iliyosababisha kuletwa mafundi kutoka Afrika Kusini, India na kadhalika:-

(a) Je, kuna *Technicians* wangapi nchini kote na katika Mikoa mingapi na ni katika hospitali zipi?

(b) Ili kuokoa fedha nyingi zinazotumiwa kwa kuleta wataalam wa nje, je, Serikali haioni kwamba litakuwa jambo la busara kuwasomesha wataalam bingwa wetu na kuwanoa wataalam hao mara kwa mara?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Janet Kahama, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa Taifa wa matengenezo ya vifaa vya tiba unahusisha vifaa katika Idara zote za ndani ya hospitali. Idara hizo ni Idara ya Radiolojia, Maabara, Upasuaji, Idara ya Macho, Mifupa, Idara ya Kinywa na Meno na Magonjwa ya Akina Mama. Mpango huo umegawanyika katika Kanda 5 kama ifuatavyo:-

Kanda ya Ziwa *(Bugando Medical Centre)* ina Mafundi 25;

Kanda ya Kaskazini *(KCMC)* ina Mafundi 20;

Kanda ya Mashariki *(Muhimbili National Hospital)* ina Mafundi 9;

Kanda ya Nyanda za Juu Kusini *(Mbeya Referral Hospital)* ina Mafundi 8; na

Kanda ya Kusini *(Ligula Hospital)* ina Mafundi 3.

Aidha, uko mpango wa kuanzisha Kanda nyingine katika Mkoa wa Tabora itakayoitwa Kanda ya Magharibi ili kupunguzia mzigo Kanda ya Ziwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba Mafundi tulionao kwa sasa wana uwezo wa kutengeneza vifaa vya tiba vyote isipokuwa vile vya Radiolojia kama *X-Ray, Ultra-Sound, MRI* na *CT-Scan*. Kwa kulitambua hilo, Wizara yangu imeandaa mpango maalum wa kutoa mafunzo kwa Mafundi wake kwa vifaa vya tiba vyote ambavyo ni vipya vinavyoingia sasa ikiwa ni pamoja na vile vya Radiolojia na Maabara ambavyo vinatumia teknolojia ya *digital*. Kwa mpango huo, Mafundi wachache watapelekwa kwenye mafunzo katika nchi ambako mashine hizo hutengnezwa ili wakirudi waweze kuwafundisha wengine.

Aidha, Wizara inawasiliana na Taasisi ya Teknolojia ya Dar es salaam *(DIT)* ili kusaidia mafunzo ya *Bio-Medical Technicians* na baadaye *Bio- Medical Engineering.* Mazungumzo yameishaanza na matumaini ya Wizara ni kuwa Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam hatimaye itaanza kutoa mafunzo haya hapa nchini. Vile vile Chuo cha Taasisi ya Tekonolojia Dar es Salaam pia kitatumika kuendesha mafunzo ya muda mfupi ili kuwaendeleza Mafundi wa vifaa vya hospitali waliopo sasa na watakaohitimu toka Chuo hicho.

**MHE. JANET B. KAHAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nilikuwa nikiangalia pia kwa upande mwingine, ni kuwa hivyo alivyozungumzia zaidi ni vile vifaa ambavyo ni kama vya *X-Ray* kama nilivyokuwa nimeulizia lakini pamoja na hivyo na vingine, vinaponunuliwa kutoka nchi za nje na vikaletwa hapa, ninaelewa vinanunuliwa kutoka nchi mbali mbali, kwa nini basi tusiwe na mpango wa kununua vifaa vinavyofanana vya *standard* moja, halafu vifaa hivyo vikawa vinatunzwa katika kituo kimoja kama vile *Central Special Equipment Services* ili kiweze ku-*monitor* na kuhakiki kuwa vifaa hivi vinatunzwa na kunagaliwa vizuri?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, vifaa ambavyo tunaingiza nchini ambavyo vinatumika katika hospitali zetu mara nyingi *MSD* inaagiza kutokana na *specification* ambazo zinaletwa na wale wahitaji wa vile vifaa vyenyewe. Sasa tukisema kwamba tulete vifaa vinavyofanana, hii sasa itakuwa ni tofauti na yale mahitaji ambayo wenyewe katika hospitali wanatutumia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninalotaka kusema ni kwamba Serikali inatambua hilo na wale Mafundi ambao watafundishwa watakuwa wanapelekwa katika maeneo yale lakini vile vile tutakuwa tunafuatisha na vinapokuja vifaa kwa sababu vinakuwa na maelezo ya jinsi ya kuvitunza vifaa vile. Kwa hiyo, tutakuwa tunafuatilia na wale Mafundi wetu watafuata *specification* na yale maelezo yanayokuja katika vile vifaa wakati vinaingizwa na baadaye kuendelea kuvifanyia matengenezo na ukarabati pale inapobidi.

Na. 83

**Tatizo la Magonjwa ya Watoto**

**MHE. JACOB D. SHIBILITI** aliuliza:-

Kwa kuwa, magonjwa hasa ya watoto wadogo yanazidi kuongezeka na kwa kuwa tiba ya watoto wadogo ni ngumu kutokana na sababu kuwa na upungufu mkubwa wa Madaktari Bingwa wa Watoto:-

(a) Je, Serikali inakabiliana vipi na magonjwa ya watoto?

(b) Je, ni hospitali ngapi za Mikoa zinazojitosheleza kwa Madaktari Bingwa wa Watoto?

(c) Je, Serikali ina mkakati upi kuhusu tatizo hili?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jacob D. Shibiliti, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeweka utaratibu wa matibabu kwa watoto kuanzia katika Zahanati, Vituo vya Afya, Hospitali za Wilaya, Mikoa na Rufaa.

Katika Vituo vyote hivi, kuna wataalam waliopatiwa mafunzo ya kutoa tiba kwa magonjwa ya watoto kupitia Mpango Maalum wa Kutoa Mafunzo kwa Tiba ya Magonjwa ya Watoto *(Integrated Management of Childhood Illnessess – IMCI)*. Mpango huu umesaidia sana katika kupunguza vifo vya watoto toka 153 mwaka 1999 mpaka kufikia 83 mwaka 2004 kwa kila watoto 1000 wenye umri chini ya miaka 5.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa hospitali za Mikoa ambazo zimejitosheleza kwa kuwa na Madaktari Bingwa wa magonjwa ya watoto ni 8 ambazo ni Hospitali ya Maunt Meru – Arusha, hospitali za Mikoa ya Kagera, Morogoro, Tabora, Ruvuma na Mkoa wa Tanga. Hospitali nyingine zenye Madaktari Bingwa ni pamoja na Hospitali ya Taifa Muhimbili, Hospitali za Manispaa za Dar es Salaam, Hospitali ya Tumbi katika Mkoa wa Pwani, KCMC - Moshi na Bugando - Mwanza.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Wizara yangu inatoa kipaumbele kwa Madaktari wanaoomba ufadhili wa Serikali katika kuchukua mafunzo ya Udhamili ili wawe Madaktari Bingwa baada ya kuhitimu mafunzo hayo. Aidha, Serikali

ina makubaliano na Serikali za Cuba na China kuleta Madaktari Bingwa kuja kufanya kazi katika Hospitali zetu za Mikoa na Hospitali za Rufaa.

**MHE. JACOB D. SHIBILITI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Kabla sijauliza, nikupongeze wewe Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ushindi wako. Lakini pia nimpongeze yeye Naibu Waziri kwa ushindi alioupata jana pamoja na Waziri wake wa Afya. Hongereni sana!

(a) Katika jibu lake Mheshimiwa Naibu Waziri amekiri kwamba bado kuna upungufu mkubwa. Lakini pamoja na upungufu huo, tatizo lingine linalowakumba Madaktari Bingwa ni pamoja na maslahi duni. Serikali ina mkakati gani wa kuboresha maslahi yao ili angalau vijana wetu waliopo kwenye shule mbalimbali au vyuo mbalimbali waweze kuhamasika kujiunga katika hospitali zetu hizo?

(b) La pili, pamoja na Madaktari Bingwa kupatikana, bado lipo tatizo kubwa la vitendea kazi katika hospitali mbalimbali. Mfano ni katika Hospitali ya Wilaya ya Misungwi, lipo tatizo kubwa la *X-Ray* pamoja na *Ultra-Sound*. Hata katika ziara ya Mheshimiwa Rais alipozungukia huko alijionea haya na akaahidi mbele ya mkutano wa hadhara kwamba litashughulikiwa haraka na akamtaja Mheshimiwa Waziri kwa jina Prof. Mwakyusa kwamba atalishughulikia upesi lakini tatizo hilo bado lipo. Je, Wizara imeshapata taarifa hiyo kutoka kwa Mheshimiwa Rais kuwa alishaahidi na hatua ikoje mpaka sasa hivi? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, napenda kushukuru kwa pongezi zake alizotupatia mimi na Mheshimiwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii na pia tunawashukuru sana Wana-CCM kwa kutupa kura hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, ni kweli kabisa kama anavyodai Mheshimiwa Mbunge kwamba moja ya tatizo ambalo linafanya tusipate Madaktari wengi ni maslahi duni. Lakini, kama ambavyo tumekuwa tukiongelea hapa Bungeni ni kwamba Serikali imekuwa ikipitia maslahi ya wafanyakazi wa Wizara ya Afya lakini vile vile maslahi ya wafanyakazi wote Tanzania nzima. Kwa hiyo, tuko katika harakati za kuweza kuona kwamba maslahi yanaboreka na tunasubiri kama Tume ilivyotoa maelezo yake basi Serikali itatekeleza ili kuboresha maslahi yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, ni kweli Mheshimiwa Rais aliona hali hii wakati wa ziara yake na alimtaja Mheshimiwa Waziri. Lakini, kama Wizara ya Afya na kama Serikali, tunalichukulia kwa ukubwa wake na tutahakikisha kwamba tunalifanyia kazi ili kuweza kuhakikisha kwamba *X-Ray* na *Ultra-Sound* zinapatikana.

Na. 84

## Sanaa ya Uimbaji Taarabu na Nyimbo za Bendi za Muziki

**MHE. HAROUB SAID MASOUD** aliuliza:-

Kwa kuwa kabla ya Uhuru, Tanganyika na Zanzibar zilikuwa miongoni mwa nchi katika Bara la Afrika zilizoanza sanaa za taarabu na nyimbo kupitia bendi zetu:-

(a) Je, ni wimbo gani wa taarabu ulio mkongwe kuliko zote ambao uko hadi sasa na ni wa mwaka gani?

(b) Je, ni wimbo gani wa bendi zetu ulio mkongwe kuliko zote ambao uko hadi sasa na ni wa mwaka gani?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO (MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Haroub, Mbunge wa Koani kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nyimbo za taarabu zilizo kongwe ziko nyingi na nyingine hazikumbukwi. Lakini zile ambazo ziko hadi sasa katika Maktaba ya Shirika letu la Utangazaji Tanzania *(TBC)* ni nyimbo tano zilizoimbwa na kikundi cha *Alwatan Musical Club* ya Dar es Salaam na kurekodiwa na Redio Sauti ya Dar es Salaam, tarehe 13 Desemba, 1955. Nyimbo hizo zinaitwa kama ifuatavyo:-

*(i) Allah walah hidar;*

*(ii) Muwar;*

(iii) Ulinikimbia kwa kuwa yetu miadi;

(iv) Hakika mpenzi ni kweli uliyoyatamka; na

(v) Bashalafu (muziki upigwao bila kuimbwa aina ya Samba).

Mheshimiwa Naibu Spika, nyimbo za bendi ya muziki wa dansi kongwe kuliko zote ambazo zipo hadi sasa katika maktaba ni nyimbo tano vile vile zilizoimbwa na *Morogoro Jazz Band.* Nyimbo hizo nazo zilirekodiwa na Sauti ya Dar es Salaam tarehe 4/3/1956. Nyimbo hizo ni kama ifuatavyo:-

(i) Mpenzi wangu tafadhali (muziki wa Rhumba);

(ii) Mpenzi sema yako niyasikie (muziki wa Samba);

(iii) Enyi wapenzi leo (Muziko wa Rhumba);

(iv) Niwe yangu wela hendewa (Kwa jina la Kiluguru);

Mheshimiwa Naibu Spika, Marehemu, Mbaraka Mwinshehe Mbaraka, aliimba kwa lafudhi ya Kiluguru; na

(v) Mpenzi ahadi imetimia (Mtindo wa Rhumba).

Mheshimiwa Naibu Spika, nyimbo hizo za taarabu na bendi za dansi zilirekodiwa baada ya kuanzishwa kwa Redio Sauti ya Dar es Salaam mwaka 1951. Kwa upande wa Zanzibar, wimbo unaojulikana kwa jina la Tamu ya Sukari, ulitungwa na kuimbwa na Bibi Siti Binti Saadi. Wimbo huo wakati huo ulirekodiwa kule Bombay, nchini India mwaka 1928.

**NAIBU SPIKA:** Kweli hapo kuna maswali ya nyongeza? *(Kicheko)*

**MHE. HAROUB SAID MASOUD:** Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali moja la nyongeza. Nimezisikia na nimeziona nyimbo ambazo zimetajwa. Lakini ukiangalia hasa nyimbo hizi nyingi ni za Tanzania Bara na kwa kuwa vile vile utamaduni wetu unaongozwa na Wizara hii; mtakubaliana na mimi kwamba Wizara inasababisha nchi yetu tuache utamaduni wetu na mfano mkubwa ni tulipoanza kuingia katika utamaduni wetu kwa kupeleka Kikundi cha Sanaa cha Tambara huko nje ambapo kilipata ushindi wa kwanza kwa sababu tuliingia katika utamaduni wetu.

Sasa kuziacha nyimbo za zamani, Wizara ikasema haina nyimbo, haina maktaba wakati nyimbo hizi ni nyingi sana mfano Elina, Nakupenda sana ambao ni wa Zanzibar, Ujanja wa Mkasi, Mpenzi wangu hawezi na Koja la Asumini, si jambo la busara. Nyimbo hizi, kama Wizara itatafuta njia ya kuzipata, inaweza ikazipata na ikaziweka katika maktaba.

Je, Wizara itakubaliana na mimi kwamba bado iko haja Wizara kutafuta nyimbo hizo kwa njia yoyote ile zihifadhiwe ili utamaduni wetu usipotee? *(Makofi/Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Sasa, afadhali mwingine naye ajaribu! Mheshimiwa Waziri mwenyewe, maana najua mnaelewana! *(Kicheko)*

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, napenda nimshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri.

Swali la msingi lilikuwa tunaulizwa nyimbo gani za zamani ambazo zinajulikana za taarabu na za bendi. Tukajibu kwamba nyimbo ziko nyingi sana na hatuzikumbuki. Lakini nyimbo ambazo zimerekodiwa rasmi ambazo ziko kwenye maktaba ni hizo ambazo tumezitaja. Hilo lilikuwa jibu la msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nyimbo ambazo amezitaja yeye za Elina na Mkasi, baadhi ya nyimbo hizi ni nyimbo ambazo zimeimbwa Zanzibar na Wizara yangu haina mamlaka ya nyimbo ambazo zimeimbwa Zanzibar, ndiyo maana hatukuziingiza hapa. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Nashukuru sana kwa majibu hayo, maana mimi nilikuwa katikati ya vurugu hapa!

Na. 85

**Suala la Vipaumbele vya Michezo**

**MHE. MZEE NGWALI ZUBEIR** aliuliza :-

Kwa kuwa Vyama vya Michezo nchini vinaulalamikia uamuzi wa Serikali wa kutoa kipaumbele kwa mchezo wa mpira wa miguu na kuviacha vyama vingine vya michezo:-

(a) Je, Serikali iko tayari kutoa vipaumbele kwa Vyama vya Michezo mingine ili kuifanya michezo yote ipate kukua nchini?

(b) Je, mchango wa michezo katika pato la Taifa ukoje katika vyama vingine vya michezo ukiacha mpira wa miguu?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO (MHE. JOEL N. BENDERA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ngwali Zubeir kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali huwa inatoa vipaumbele kwa Vyama vya Michezo mingine nchini kama ilivyo kwa mchezo wa mpira wa miguu ili iweze kukua na kuendelezwa. Ili kuendeleza azma hiyo, Wizara kupitia Idara ya Maendeleo ya Michezo na Baraza la Michezo la nchi, imeandaa mikakati thabiti mipya ya kusaidia kukuza na kuendeleza michezo hapa nchini. Baadhi ya mikakati hiyo ni pamoja na:-

- Kufufua mashindano ya michezo mbalimbali kwa watoto wenye umri mdogo katika shule za msingi, sekondari na vyuo, kwani michezo mashuleni ndiyo

msingi wa kuendeleza vipaji vya wanamichezo katika michezo ya aina zote. Upo usemi usemao "Samaki mkunje angali mbichi".

- Kutoa mafunzo kwa Walimu, Makocha na Waamuzi wa michezo mbalimbali katika vyuo vyetu vya Serikali vya Mallya, Butimba vilivyo Mkoani Mwanza.

- Kuhimiza watu binafsi kuanzisha shule za michezo kwa watoto *(Sports Academies)* ili kuibua vipaji mbali mbali na kuviendeleza.

- Kuhimiza vyama vya michezo, kuendesha na kutoa mafunzo ya Walimu, Makocha na Walimu wa michezo mbalimbali katika nchi yetu.

- Dhamira yetu ni kuwa na viwanja vya kisasa vyenye viwango vinavyokubalika Kimataifa vya michezo mbalimbali Mikoani na Wilayani ili vitumiwe na wanamichezo wetu.

- Kuandaa mfumo wa katiba za vyama vya michezo utakaoweka bayana taratibu za uendeshaji wa vyama na vilabu kwa maslahi ya wanachama na wadau wa michezo kwa faida ya Taifa zima kwa ujumla ili kuondoa migogoro.

- Kuhamasisha taasisi mbalimbali kama vile Wizara, Mashirika ya Umma, Majeshi ya Ulinzi na Usalama na makampuni binafsi kulipa kipaumbele suala la michezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiachia mpira wa miguu, michezo katika vyama mingine vya michezo, huchangia pato la Taifa:-

- Michezo hujenga afya na akili kwa watu ili waweze kufanya kazi iletayo tija na kuongeza pato la Taifa.
- Michezo huleta upendo na ushirikiano katika Taifa ambalo watu wake huweza kuzalisha mali kwa amani na utulivu

- Wanamichezo wetu wanaoshinda katika mashindano ya mbio ndefu kama vile *Marathon* hupata Dola za Marekani kwa viwango tofauti. Fedha hizo huja kutumika hapa nchini kwetu na hivyo kuwa sehemu ya pato la Taifa.

- Michezo huendeleza utalii pale ambapo wanamichezo kutoka nje ya nchi wanapofika hapa nchini kushiriki mashindano mbalimbali kama vile mbio za *Kilimanjaro Marathon* ambazo zinafanyika kila mwaka, mashindano ya *Handball*, Mashindano ya *Basketball*, mashindano ya *Netball*, Mashindano ya *Rugby* na kadhalika.

**MHE. MZEE NGWALI ZUBEIR:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Lakini naona kama kalipiga chenga hili swali. Swali langu lilikuwa linasema kwa nini vipaumbele zaidi inapewa *football* kuliko vyama vingine vya michezo? Hakulijibu ipasavyo! Nataka kumuuliza, je, anaweza kunionyesha bajeti ya vyama vyote vya michezo ili tuhakikishe kuwa kweli kipaumbele kipo katika vyama vingine vya michezo?

Pili, kwa nini wahisani wengi tunawasukuma kwenye *football* kuliko vyama vingine na tukaweka sawa hii michezo mingine ili ieleweke na ifahamike katika nchi nzima?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO (MHE. JOEL N. BENDERA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nataka nisikubaliane naye kwamba sikulichenga swali, liko wazi kabisa. Naomba niondoe dhana potofu iliyoko kwa wananchi wengi kwamba Serikali inapendelea sana mpira wa miguu, si kweli! Serikali inaendeleza michezo yote na hata katika bajeti yetu ya mwaka huu mmeona hatukuzungumzia mpira wa miguu, tumezungumzia maendeleo ya michezo kwa ujumla na ndiyo mana hata swali lake limelenga huko. Kawaida ilivyo, ni kitu ambacho hakipingiki, hapa nina majina ya nchi nyingine duniani na nchi za Afrika 42, wameweka kipaumbele mpira wa miguu kwa sababu ni mchezo ambao unapendwa na wengi. Sasa ni *automatic* tu kwamba ni mchezo ambao ni rahisi, unachezwa hata barabarani, *one against one* barabarani watu wanacheza, tofauti na michezo mingine. Katika bajeti yetu sisi hatukuweka kwamba mpira wa miguu shilingi kadhaa, *basketball* shilingi kadhaa, *handball* shilingi kadhaa, tumeweka michezo yote kwa ujumla na yote tunaiendeleza inavyostahili, hatukutoa upendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili, ni ukweli kwamba wale wanaojitolea wahisani au wafadhili wote tunawahamasisha sawa wapende michezo yote lakini wao wenyewe wanapenda kusaidia mpira wa miguu. Cha kufurahisha tu ni kwamba hivi karibuni wengine wameanza kujitokeza, *Barrick* kwa mfano, wamejitolea ama wameamua kusaidia *Basketball*. Hata mashindano ya juzi ya *Basketball* yamedhaminiwa na *Barrick*. *Easy Finance* wamesaidia kufadhili *handball*, *Easy Finance* wamefadhili ngumi na wengine wanajitolea kudhamini michezo mingine. Lakini mchezo wa mpira wa miguu unapendwa na wenyewe. Huwezi kumwambia mfadhili naomba udhamini *Basketball*, atakwambia sitaki, nataka mpira wa miguu, utamwabia sitaki! Huwezi!

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kama unavyojua bajeti yetu ya Wizara hii ni ndogo sana kwa kulinganisha na bajeti za Wizara yoyote ile. Tumepewa milioni 90 kwa ajili ya *International participation*. Milioni 90 ni nauli ya kupeleka timu Zaire na kurudi. Kwa hiyo, tunategemea wafadhili ili watusaidie na wanapoamua kutusaidia, hatuwalazimishi waende kwenye *basketball*, waende kwenye *Netball*, waende kwenye riadha. Tunaomba mfadhili yeyote ajitokeze na huu ni wito natoa kwa michezo yote. Hata Waheshimiwa Wabunge, tusaidieni wafadhili wa michezo mingine, siyo mpira wa miguu tu na Serikali haiko kwa ajili ya mpira wa miguu tu, lakini mpira wa miguu unapendwa. *(Makofi)*

**MHE. MWANAWETU SAID ZARAFI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante! Mimi nina swali dogo tu la nyongeza.

Kwa kuwa Serikali iko tayari kusaidia michezo yote bila kubagua na kwa kuwa hivi karibuni Timu ya Mpira, *Taifa Stars*, ililetwa Bungeni kwa ajili ya kuja kuipongeza kwa ushindi na kuipa motisha ya kuweza kuendelea na mchezo, je, ni vipi itakuwa kwa timu zile ambazo pia zimeleta ushindi hapa Tanzania, mfano Mabondia au Timu ya Walemavu ambayo imeleta ushindi mkubwa hapa Tanzania? Ni lini Serikali itafikiria kuwaleta hapa Bungeni na wenyewe wakapongezwa kama ilivyopongezwa Timu ya Mpira wa Miguu? Ahsante!

**NAIBU SPIKA:** Kutokea kuchangia hadi kupongezwa.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO (MHE. JOEL N. BENDERA)**: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwanawetu, kama ifuatavyo:-

Nakubaliana na mawazo yake lakini si kila wanamichezo wanaoshinda tuwalete Bungeni, itakuwa ni vichekesho, si kila anayeshinda aje Bungeni, kuna *priorities*. Tumekwishawaleta watu wa riadha na juzi kwa bahati mpira wa miguu kwa sababu yalikuwa ni mashindano makubwa na mazito. Wananchi walikuwa wamehamasika, kwa hiyo, na Waheshimiwa Wabunge wakaona angalau wafike, lakini hatukatai itakapotokea na tukiweza kuweka mipango mizuri tunaweza kuwaleta hao walemavu. Napenda niishukuru Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii kwa kazi nzuri waliyofanya kuwaita Dodoma ndani ya Bunge juzi na kuwapongeza, hiyo inatosha.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nashukuru sana, maswali yamekwisha na muda umefika, sasa napenda niwatambue wageni wetu walioko ndani ya Bunge.

Kwanza kabisa, napenda nimtambue Mheshimiwa Joseph Sinde Warioba na Mke wake, wamekuja kututembelea. Alikuwa Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais, kipindi cha miaka ile ya themanini mpaka Tisini na mimi ndiye alikuwa bosi wangu, kwa hiyo, karibuni sana.

Pia naomba niwatambue, sijui kama wamekwishaondoka, kuna ujumbe wa maafisa kutoka Balozi mbalimbali tunaofanya nao kazi, sijui kama wapo. Yupo Theo Kaspaz kutoka *European Commission*, tunae Victor Masinde, kutoka *UNDP*, *they are all there*, kuna Kiiza Kensten kutoka *European Commission*, kuna Olive Nagley kutoka *Irish Embassy*, kuna John Brandshow kutoka *British High Commission*, kuna Andres Estima kutoka *Swedish Embassy* na kuna Kitama Joseph kutoka *Swedish Embassy*. *I have had some discussions with you again , you are welcome!*

Halafu tuna Wabunge watatu kutoka Namibia sijui kama wapo, nafikiri wametoka lakini walikuwepo wageni watatu kutoka Namibia, nadhani kesho

watakuwepo. Halafu tuna Mheshimiwa Lubeleje, ana wageni wake, yupo Mkuu wa Wilaya ya Mpwapwa, Mheshimiwa Halima Mdendego, yuko wapi Mheshimiwa *DC*? Kuna Mheshimiwa Fikirini Masokola, Katibu wa CCM, Wilaya ya Mpwapwa, kuna Mheshimiwa Honorata Pima, Mwenyekiti wa CCM, Wilaya ya Mpwapwa, na wajumbe wengine waliofuatana nao, tunaomba wote wasimame na karibuni. *(Makofi)*

Pia nina wageni kutoka Idara ya Sheria ya Ubalozi wa Marekani, wanaweza kusimama walipo. *I think they have gone out,* wamekwenda kufanya kazi zingine. Halafu nina wageni wa Mheshimiwa Salum, Mbunge wa Meatu, kama wapo wasimame wote, karibuni sana! Nina wageni wa Mheshimiwa Shah, Katibu wa Uchumi na Fedha, Wilaya ya Mafia, kumbe wako wengi, karibuni sana!

Kuna wageni wa Mheshimiwa Michael Laizer, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Longido, Mkurugenzi wa Maendeleo Wilaya hiyo hiyo karibuni sana! Kuna mgeni wa Mheshimiwa Chiligati, lakini pia huyu mgeni ni Baba yake aliyekuwa Katibu wa Bunge, Jaji Kipenka Mussa na ni muasisi wa Chama cha Mapinduzi, Mzee Rev. Thomas Mussa, nafikiri kwa ajili ya utu uzima ametoka, tunamkaribisha.

Tulikuwa na Mheshimiwa Spika Mstaafu, Pius Msekwa, bahati mbaya ametoka kabla hatujafikia muda wa kutambulisha wageni lakini lengo na madhumuni yake ya kuja hapa alikuwa anapenda kutoa shukrani zake za dhati kwa Waheshimiwa Wabunge kumpa kura zote na kumwombea kura kwa Wajumbe wa Mkutano. Kwa hiyo, kwa niaba yake naomba mpokee ujumbe huo.

Baada ya hapo nilikuwa na matangazo ya kazi. Kwanza kabisa Mheshimiwa Estherina Kilasi anawatangazia Wabunge wa CCM wafike Chumba Na. 106 baada ya maswali haya. Wabunge wa CCM ambao wengine hawakwenda katika chumba kile waende, sio wote ni wale ambao hawakwenda.

Halafu Mheshimiwa Shellukindo, yeye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Uwekezaji, anawatangazia wajumbe wa Kamati wakutane saa 7.00 mchana katika ghorofa ya pili, chumba namba 219. Kuna mkutano labda baada ya tangazo lingine ataamua kubadilisha kwa sababu tuna nia ya kuahirisha kikao sasa hivi. Sasa kama unataka kubadili saa badilisha, tunaahirisha mpaka jioni, wakutane baada ya kumaliza mkutano huu chumba kile kile.

Pia Mheshimiwa John Cheyo, Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali anawatangazia wajumbe wake wakutane chumba namba 231 sijui ni sasa hivi au mpaka saa 7.00?

**MHE. JOHN M. CHEYO**: Mheshimiwa Naibu Spika, kama inawezekana badala ya saa 7.00, wajumbe tukutane tangu saa 5.00 baada ya chai.

**NAIBU SPIKA:** Halafu pia tunafurahi kwamba wabunge kumi ambao walikuwa wamekwenda Misri kwa mafunzo maalumu, wamerejea na nafikiri Waziri wa Nchi, Mheshimiwa Dr. Batilda Buriani alikwenda kule akawa amefanya mawasiliano na

wahusika kwamba utaratibu wa kuwapeleka kwenye mafunzo Misri utakuwa endelevu kwa kipindi fulani. Kwa hiyo, kundi la kwanza limerudi halafu litapatikana na kundi lingine kadri litakavyokuwa linapangwa.

Waheshimiwa Wabunge, wajumbe wa Kamati ya Mheshimiwa Lubeleje pia wanatakiwa wakutane, sijaona karatasi yake!

Waheshimiwa Wabunge, katika *Order Paper* yetu mtaona kwamba tulikuwa tunafuatiwa na muswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria ya Baraza la Ujenzi ya Taifa mwaka 2007. Muswada huu wamejitokeza wadau ambao ni wahusika sana, wangependa kuwa na *inputs* katika muswada huu.

Kwa sababu muswada wowote tunapoutunga lengo letu ni kwamba uwe na manufaa kwa wadau na wananchi, sasa hawa wame-*express* wenzetu wengine kwamba wangependa kuongeza ubora wa muswada huu kupitia Kamati na Wizara inayohusika.

Kwa hiyo, tunaona tuuaharishe sasa mpaka saa 11.00, wadau watakutana baada ya kikao hiki, wataupitia huu tena na saa 11.00 tutaendelea na kuupitia muswada huu, hivyo saa 11.00 mrudi.

Ni kwa sababu tuna watu wengine ambao ni wadau sana, wangependa kutoa maoni yao hapa, kwa sababu hawakupata muda Dar es Salaam lakini wamekuja hapa. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni.

*(Saa 4.40 Asubuhi Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

## MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI.

### Muswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria ya Baraza la Ujenzi la Taifa wa Mwaka 2007 *(The National Construction Council (Amendment) Bill 2007)*

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**MHE. JOB Y. NDUGAI- MWENYEKITI**: Waheshimiwa Wabunge, kama mtakumbuka, asubuhi Mheshimiwa Naibu Spika, alielezea kutokuwa tayari kwa suala zima linalohusiana na Muswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria ya Baraza la Ujenzi la Taifa wa mwaka 2007.

Naomba niwaarifuni kwamba bado zoezi hilo halijakamilika, bado Kamati haijamaliza kazi zake. Kwa hiyo basi, naomba kuwatangazia Wajumbe wote wa Kamati inayohusika, nadhani ni Kamati ya Miundombinu, muda si mrefu wakaendelee na shughuli yao, wamalizie mambo haya. Kwa sababu hiyo mezani kwangu hakuna shughuli nyingine mpaka shughuli zote zitakapokuwa zimekamilika kwa maana ya kuziingiza katika Bunge letu.

Kwa hiyo basi, naomba nichukue fursa hii kuahirisha shughuli za Bunge hadi kesho 3.00 Asubuhi.

*(Saa 11.04 jioni Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumatano,*
*Tarehe 7 Novemba, 2007, Saa 3.00 Asubuhi)*